# KISIWA CHA RHODE

## Programu ya Vichocheo vya Ubora wa Mazingira (EQIP)



Mazoea ya Uhifadhi ya NRCS (kutoka juu hadi chini): Vijia Vikubwa vya Chini ya Ardhi, Mipango ya Malisho, Makazi ya Kichavushi, Kupunguka kwa Misitu, Kuweka Uzio wa Malisho kwa ajili ya Malisho Yanayofuata Maagizo, Kukata Maeneo Mahususi ya Misitu, Mifumo ya Umwagiliaji Maji Mashambani.

Programu ya Vichocheo vya Ubora wa Mazingira (EQIP) ni programu ya kujitolea inayotoa msaada wa kiufundi na kifedha kwa wakulima na wamiliki wa ardhi ya misitu ambao wangependa kuboresha na kulinda udongo wao, maji, hewa, mimea na wanyama.

## MANUFAA ya EQIP

- Washiriki wanaweza kupokea msaada wa kifedha na kiufundi ili kutumia mazoea ya uhifadhi ya kimuundo na usimamizi ili kushughulikia wasiwasi wa rasilimali asili.
- Uzalishaji ulioboreshwa na afya jumla ya mfumo wa ikolojia kwenye ardhi za kilimo na ardhi ya misitu.
- Ubora ulioboreshwa wa rasilimali asili.

## MAZOEA ya Kawaida

*Je, kuna yoyote kati ya yafuatayo yanasikika kuwa mambo mazuri kwako?*

- Mipango ya Kina ya Usimamizi wa Virutubisho
- Udhibiti wa Mmomonyoko
- Mipango ya Misitu
- Kuboresha Hali ya Misitu
- Ulinzi wa Maeneo yenye Matumizi Makubwa
- Vijia Vikubwa vya Chini ya Ardhi
- Mifumo ya Umwagiliaji Maji Mashambani
- Upanzi wa Malisho na Mashamba ya Nyasi
- Kuweka Uzio wa Malisho
- Makazi ya Kichavushi
- Malisho Yanayofuata Maagizo
- Kupunguka kwa Misitu
- Maeneo salama kando ya Mito
- Vituo vya Uhifadhi wa Taka
- Makazi ya Wanyama Pori

## WASILISHA MAOMBI ya Kufadhiliwa

- Wasiliana na RI NRCS kupitia 401-828-1300 au Wilaya ya Uhifadhi ya eneo lako (tazama habari iliyo hapa nyuma).
- Jaza fomu ya Kuwasilisha Maombi ya EQIP.
- Wasilisha fomu hii katika ofisi ya eneo lako ya NRCS.

**RI NRCS**
**60 Quaker Lane, Suite 46**
**Warwick, RI**
**401-828-1300**
**www.ri.nrcs.usda.gov**







Mazoea ya Uhifadhi ya NRCS (kushoto hadi kulia): Makazi ya kichavushi, Mipango ya Usimamizi kwa ajili ya uzalishaji ulioboreshwa wa mifugo, Usimamizi wa Misitu.

**Mashamba ya mimea ♦ Malisho ♦ Mashamba ya nyasi ♦ Mashamba ya misitu**

## Jambo la KUTARAJIA wakati unawasilisha maombi

- Mawasiliano na Mpangaji wa Uhifadhi.
- Utathmini mwafaka — ikijumuisha **ziara kwenye eneo** ili *kuorodhesha* rasilimali asili zilizopo, *kutambua* wasiwasi wa rasilimali na *kujadili* malengo na madhumuni yako ya muda mrefu ya ardhi yako.
- Mpango wa Uhifadhi uliotengenezwa na Mpangaji.
- Nafasi ya maombi yako kupitia mfumo wa kuorodhesha wa nchini kote.
- Kutengenezwa kwa kandarasi kulingana na alama ya nafasi yako na fedha zilizopo.

## VIDOKEZO Muhimu—piga simu ili kujua zaidi!

- Maombi yanaweza kuwasilishwa wakati wowote katika mwaka.
- Fedha zilizopo husambazwa katika muda mbalimbali katika mwaka, kulingana na mfumo wa kuorodhesha wa nchini kote.
- Kuorodheshwa huendelea hadi fedha zote za EQIP zinapowajibishwa.
- Ufadhili wa EQIP umeidhinishwa na Mswada wa Shamba wa 2018.
- Mazoea yanayofadhiliwa yanaweza kutambuliwa kila mwaka na ofisi ya Kitaifa ya USDA-NRCS.
- Wakulima wasiohudumiwa ipasavyo kihistoria (walio na rasilimali finyu, wanaoanza ukulima, wasiopendelewa kijamii, Makabila) wanaweza kustahiki viwango vya malipo ya mazoea vya juu zaidi ili kutekeleza mazoea na mipango ya uhifadhi.

♦ ♦ ♦

**Wilaya za Uhifadhi za Eneo lako ziko tayari kukusaidia!**


### Eastern RI Conservation District

*Inahudumia Kaunti za Newport na Bristol*

401-934-0842 or info@easternriconservation.org

### Northern RI Conservation District

*Inahudumia Kaunti ya Providence*

401-934-0840 or mallard.nricd@gmail.com

### Southern RI Conservation District

*Inahudumia Kaunti za Kent na Washington*

401-500-0422 or gfuller@sricd.org


USDA Inatoa Fursa Sawa za Uhudumu, Uajiri na Ukopeshaji.